

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BUNGE LA TANZANIA

Simu: +255 26 2322761-5  
Fax No. +255 26 2324218  
E-mail: cna@bunge.go.tz



Ofisi ya Bunge,  
10 Barabara ya Morogoro,  
S. L. P. 941,  
40490 Tambukareli,  
DODOMA

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Katibu wa Bunge anatoa Taarifa kwa Umma kwamba Uchaguzi wa Wajumbe Watatu (3) watakaojaza nafasi zilizo wazi za kuiwakilisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki utafanyika katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa Mkutano wa Tatu wa Bunge unaoendelea Jijini Dodoma.

Nafasi hizo zilizo wazi mbili ni za Kundi la Wagombea Tanzania Bara na nafasi moja ya Kundi la Wanawake, ambapo zote ni kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM).

Pamoja na Taarifa hii, Katibu wa Bunge ambaye ndiye Msimamizi wa Uchaguzi huo, atatoa Tangazo kwenye Gazeti la Serikali kwa mujibu wa masharti yanayohusu siku ya uteuzi, ambayo ni tarehe 30 Aprili, 2026 saa kumi kamili jioni (10:00) na pia kuhusu siku ya uchaguzi ambayo ni tarehe 4 Mei, 2026 saa Tano kamili asubuhi (05:00) mara baada ya Kipindi cha Maswali.

Aidha, katika Tangazo hilo, Katibu wa Bunge atatoa masharti yanayopaswa kuzingatwa na wagombea wa chama cha siasa ambacho kina sifa ya kujaza nafasi za wajumbe kwa ajili ya kukiwezesha kuanza mchakato wa kuwapata wagombea kupitia chama hicho, ambao majina yao yatawasilishwa Bungeni kwa ajili ya kupigiwa kura.

Kwa taarifa hii, watu ambao wanazo sifa za kugombea na kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki Kundi la Wagombea Tanzania Bara na Kundi la Wagombea Wanawake wanaweza kuanza mchakato wa kuteuliwa kushiriki katika uchaguzi huo kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM).



---

Chama au wagombea walioshinda katika ngazi ya chama wanapaswa kujaza Fomu ya Uteuzi kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza na kuiwasilisha kwa Katibu wa Bunge. Fomu hiyo itatangazwa katika Gazeti la Serikali na inapatikana kwenye Tovuti ya Bunge ambayo ni [www.bunge.go.tz](http://www.bunge.go.tz).

**Imetolewa na:** Kitengo cha Mawasiliano na Elimu kwa Umma,  
Ofisi ya Bunge,  
**DODOMA.**

**14 Aprili, 2026.**

